
# Jinsi serikali ilivyojipanga kwa uwekezaji mifugo, uvuvi



BAADHI ya washauri wa mifugo kutoka mikoa mbalimbali nchini, waliohudhuria kikao kazi, kilichofanyika mkoani Singida hivi karibuni.

**Na NATHANAEL LIMU,SINGIDA**

UTEUZI wa mawaziri na naibu mawaziri, awamu hii ulichukua muda kutangazwa. Rais Dk. John Magufuli alilazimika afanye hivyo, kwa kuwa kulikuwa na kundi kubwa la Watanzania wenye sifa za kushika nafasi hizo, Hivyo kulihitajika umakini mkubwa na muda wa kutosha.

Baada ya chujio kupita, Rais aliamua kuteua majembe ya uhakika ambapo Watanzania waliowengi walipongeza uteuzi huo.

Baada ya kuawaapisha rasmi wateule wakie Desemba mwaka jana katika Ikulu ya Chamwino jiji la Dodoma, Rais aliwaagiza wakafanye kazi kwa weledi, wawe viongozi wa kuchukua uamuzi kwenye nafasi zao. Lengo kuu likiwa ni kuhakikisha Ilani ya uchaguzi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) 2020/2025, inatekelezwa kama ilivyokusudiwa.

Aliagiza mawaziri hao wawe wabunifu na wenye maono ya mbali. Na wasisubiri hadi Rais awaelekeze nini cha kufanya.Wajiamini katika uamuzi wao.

Baada ya kuapishwa wizara ya mifugo na uvuvi, haikuchelewa kuanza kutekeleza maagizo ya Rais Magufuli, Wizara hiyo ilifanya kikao kazi kilichohudhuriwa na wataalamu washauri wa mifugo katika mikoa yote nchini. Kikao hicho kilichofanyika mjini Singida, pia kilihudhuriwa na wataalamu wa wizara ya mifugo na uvuvi.

Baadhi ya viongozi wa juu wakiwemo Mkurugenzi Mratibu wa Sekta Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mkurugenzi wa Utafiti Mafunzo na Ugani (DRTE), Mkurugenzi wa Uzalishaji na Masoko (DPM), Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo (DVS), Mkurugenzi wa Rasilimali za Malisho na Vyakula vya Mifugo (DGLF). Na wakuu wa vitengo wa wizara ya mifugo na uvuvi na sekta ya mifugo, walihudhuria kikao hicho.

Akifungua kikao hicho, Katibu Tawala Mkoa wa Singida Dk. Angelina Lutambi, alisema sekta ya mifugo ni miongoni mwa sekta za kiuchumi ambayo, ni muhimu katika kuondoa umaskini na kukuza uchumi wa Taifa kwa ujumla.

"Sekta hii inachangia katika kuwapatia wananchi ajira, chakula,lishe, kipato na fedha za kigeni. Katika mwaka wa 2019/2020 sekta hii, imechangia asilimia 7.4 katika pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 7.2 ya mwaka 2018/2019.

Sekta imekuwa kwa asilimia tano kwa mwaka 2019/2020 ikilinganishwa na asilimia 4.9 mwaka 2018/2019,", amesema.

Katika hotuba yake iliyosomwa kwa niaba yake na Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Deogratuas Yinza, alisema mafanikio hayo yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na juhudi za maofisa mifugo, wafugaji na wadau wengine katika kufanya kazi kwa bidii. Lengo likiwa ni kuzalisha kwa tija.

Alisema wafugaji wakipata huduma bora za ugani, huduma hizo zitachochea ongezeko la uzalishaji wa malighafi za viwandani zitokanazo na mifugo. Pia zitakuwa chachu ya safari ya ongezeko ukuaji wa uchumi.

"Ipo fursa kubwa ya sekta ya mifugo kuchangia zaidi katika pato la mfugaji binafsi na taifa kwa ujumla endapo fursa zitafumka vizuri.

Fursa hizo ni pamoja na uwepo wa mahitaji ya malighafi za mifugo kwenye viwanda vya kusindika mazao ya mifugo vinavyojengwa sehemu mbalimbali hapa nchini. Na upatikanaji wa mbegu bora za mifugo na pembejeo nyingine,"alisema.

Fursa hizo ni pamoja na uwepo wa mahitaji ya malighafi za mifugo kwenye viwanda vya kusindika mazao ya mifugo vinavyojengwa sehemu mbalimbali hapa nchini. Na upatikanaji wa mbegu bora za mifugo na pembejeo nyingine

Dk.Lutambi alisisitiza kwamba katika majadiliano yao na kubadilishana uzoefu, wapeane elimu na maarifa mapya ambayo anaamini yatasaidia kuinua sekta ya mifugo.

"Wizara imeainisha mikakati ambayo inaendana na sera za serikali na inaendana na Ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM). Najua kwamba mikoa inatekeleza majukumu mbalimbali ya sekta kuendana na utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM, ahadi za Rais Dk. Magufuli anazitoa kwa nyakati tofauti katika hotuba zake mbalimbali.

Hivyo nichukue nafasi hii kuwahamasisha wote kutumia kikao kazi hiki, ili kujadili na kutengeneza maazimio ambayo yatatekelezeka kwa ushirikiano wa wizara zetu za sekta na Ofisi ya Rais TAMISEMI,"alisema Dk.Lutambi.

Alieleza kwamba baada ya majadiliano hayo, matarajio yake ni kuwa watapata maarifa mapya yatakayotumika kupanga mipango ya maendeleo ya tasnia ya mifugo.

"Baada ya kikao hicho nendeni mkahamasishe ufugaji wa kisasa na kibiashara katika mikoa yenu.

Mkatambue changamoto na fursa zilizopo kwenye sekta ya mifugo, ili kuhamasisha uwekezaji kwenye mikoa yenu. Wizara na wataalamu wa mifugo mtaendelea kushirikiana, ili kuzipatia majawabu changamoto zinazoikabili sekta ya mifugo.

Kwa lengo la kutimiza azma ya serikali ya awamu ya tano ya uchumi wa viwanda," alisema.

"Naomba wizara ikishirikiana na OR TAMISEMI na sektaretarieti za mikoa yote, kuona namna nzuri ya kufanya ufuatiliaji na tathimini kila mwaka.

Ili kuhakikisha utekelezaji wa ilani ya CCM, hotuba ya Rais Magufuli na ASDP II imetekelezwa kwa kiwango kilichokusudiwa,".

Awali Kaimu Mkurugenzi Idara ya Utafiti Mafunzo na Ujenzi Wizara ya Mifugo na Uvuvi Dk.Kejeli Gillah, alisema kitakachotolewa na kikao hicho, ndicho kitakachotumika kuandaa bajeti ya 2021/2022.

Anasema anaamini kwamba baada ya kikao hicho, mageuzi makubwa yanaenda kufanyika, ikiwemo ufugaji utakao kuwa wa tija zaidi.

Dk. Gillah alisisitiza kwamba kila kiongozi aliyehudhuria kikao hicho, ahakikishe anatoka na mawazo mapya ya namna gani atasaidia wafugaji kufuga kisasa na kibiashara.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi Huduma za Mifugo Nchini, Dk. Stanford Ndibalema amezitaka halmashauri za wilaya, manispaa na majiji, zitekeleze waraka namba moja uliotolewana Rais mwaka 2001, unaoelekeza kutenga bajeti kwa ajili ya kuhudumia mifugo.

"Fedha za bajeti hiyo,zitokane na asilimia 15 ya fedha zote za tozo za mazao mbalimbali ya mifugo na zielekezwe katika kugharamia uboreshaji/ujenzi wa majosho, minada na chanjo mbalimbali. Pia zitumike kugharamia shughuli za ustawi wa ufugaji mifugo na uvuvi,"alieleza.

**"Fedha za bajeti hiyo,zitokane na asilimia 15 ya fedha zote za tozo za mazao mbalimbali ya mifugo na zielekezwe katika kugharamia uboreshaji/ujenzi wa majosho, minada na chanjo mbalimbali. Pia zitumike kugharamia shughuli za ustawi wa ufugaji mifugo na uvuvi,"**

Kaimu Mkurugenzi Huduma za Mifugo Nchini, Dk. Stanford Ndibalema

### ZAO LA NGOZI

Ofisa Mifugo Mkoa wa Mara, Denis Ishegoma, alisema zao la ngozi linahitaji kuboreshwa, ili liweze kukidhi mahitaji ya kiwango cha ndani na nje ya nchi.

"Zao la ngozi ni zao kama mazao mengine, na lina uwezo wa kumkomboa mfugaji kiuchumi. Ngozi bora itamwingizia mfugaji kipato kizuri na Taifa litapata mgao wake.

Elimu juu ya upatikanaji wa ngozi bora, inahitajika. Kule kwetu Mara, ngozi nyingi hutupiwa mbwa. Ni vema elimu kuanzia ngazi ya chini yaani wafugaji ikatolewa. Ili wafugaji waweze kuwa na utamaduni wa kutambua ngozi bora, waache kuzitoboa au kuweka alama zisizo na umuhimu wo wote,"alisema.

Naye Daktari wa Mifugo Mkoa wa Morogoro Gasper Msibe, aliwataka wachunaji wakiwemo wa machinjioni, wawe ni wale walipata mafunzo, na si vinginevyo.

Alivitaka viwanda vya ngozi viwe na mawakala ambao watanunua ngozi bora kwenye halmashauri. Pia alishauri ngozi ziwe zinapangwa kwa madaraja kabla ya kupelekwa sokoni.

### MKAKATI WA UTEKELEZAJI

Baadhi ya mikakati hiyo, ni pamoja na lengo la kuongeza uzalishaji wa mazao yatokanayo na mifugo. Mazao hayo ni maziwa kutoka lita bilioni 2.7 hadi wastani wa lita bilioni 4.5. Nyama nyekundu kutoka tani 690,629 hadi tani 790,000.

Imeelezwa ili kufikia lengo hilo, ni lazima kazi ifanyike ya kuhamasisha wafugaji katika halmashauri zote nchini. Kuboresha mifugo kwa kutumia, mbengu bora za mifugo. kuboresha huko kupitia uhimilishaji, uhawiliahaji, kiini tete na upandishaji madume bora.

Kwa upande wa mikoa, itakuwa na majukumu ya kuhamasisha na kusimamia uzalishaji wa ng`ombe wa maziwa, kwa kuongeza idadi ya ng`ombe wa maziwa kutoka milioni 1.5 hadi milioni tatu (03) kupitia uhimilishaji wa madume.

Lengo jingine ni kuongeza uzalishaji wa mazao yatokanayo na mifugo yakiwemo ya nyama nyeupe kutoka tani 82,500 hadi tani 150,000. Mayai kutoka bilioni 3.6 hadi bilioni 5.

Lengo hilo litafikiwa kwa kuhamasisha uanzishwaji mashamba ya kuku wa asili na wa biashara. Na vituo vya kutotolesha katika vijiji vitano (05) kwa kila wilaya.

Pia kuhamasisha ufugaji wa kuku na sungura katika shule za msingi, sekondari na vyuo vya ufundi hapa nchini.

Mikoa itafuatilia na kusimamia uanzishwaji mashamba ya kuzalisha kuku katika mkoa. Kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa ufugaji kuku na sungura katika shule za msingi, sekondari na vyuo vya ufundi na kusimamia na kufuatilia ujenzi wa machinjio za kisasa.

Tanzania ni ya pili kwa mifugo mingi bara la Afrika, ikitanguliwa na Ethiopia. Tanzania inakadiriwa kuwa na ng'ombe milioni 33.4, mbuzi milioni 21.29, kondoo milioni 5.65, kuku wa asili milioni 38.77, kuku wa kisasa milioni 44.51, nguruwe milioni 2.14 na punda 657,389.

Scanned with CamScanner

# Bil 8/- kuboresha biashara migebuka, dagaa

Na Gloria Tesha


TANZANIA ni miongoni mwa nchi 10 kati ya 79 za Jumuiya ya Nchi za Afrika, Caribbean na Pacific (OACPS), zilizochaguliwa kunufaika na mradi wa zaidi ya Sh bilioni nane (Euro milioni tatu) kwa ajili ya kuongeza mnyororo wa thamani wa samaki.

Mradi huo kupitia Mfuko Maalumu wa Maendeleo wa Umoja wa Ulaya (EDF11 for Intra-ACP Projects), utatekelezwa mkoani Kigoma kwa kipindi cha miaka mitano na unahusu samaki aina ya migebuka na dagaa kutoka Ziwa Tanganyika.

Taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa jana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ilieleza kuwa Tanzania imechaguliwa kunufaika na mradi huo wa thamani zaidi ya Sh bilioni nane.

"Mradi huo utatekelezwa mkoani Kigoma kwa kipindi cha miaka mitano na kusimamiwa na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (Tafiri) ambapo wavuvi wadogo watapatiwa ujuzi wa kuongeza uzalishaji.

"Watasaidiwa kupunguza upotevu wa mazao ya samaki, kuwezesha mazao ya samaki kufika kirahisi katika masoko ya ndani na n je na utunzaji wa mazingira kuwezesha uvuvi endelevu na wenye tija," ilieleza taarifa hiyo.



Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Tanzania ni miongoni mwa nchi 10 kati ya 79 za OACPS zilizochaguliwa kutekeleza mradi huo, unaojulikana kama Fish-4ACP utakaotekelezwa kwa gharama ya Euro milioni 40 kupitia mfuko wa EDF11 wa miradi ya Intra-ACP.

Mbali na Tanzania, nchi nyingine kwa upande wa Afrika ni Cameroon, Ivory Coast, Nigeria, Sao Tome, Senegal na Zimbabwe. Kwa upande wa Caribbean na Pacific ni Jamhuri ya Dominica, Guyana na Visiwa vya Marshall.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa kupatikana kwa mradi huo ni utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli wakati akizindua Bunge la 12 alipoagiza Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kupitia Balozi za Tanzania nje ya nchi, kuhakikisha sekta ya uvuvi inatoa mchango katika kukuza pato la Taifa, ajira na kupambana na umasikini.

"Serikali ya Tanzania kupitia ubalozi wa Tanzania nchini Ubelgiji imeomba kibali kutoka Umoja wa Ulaya kuruhusu dagaa wa Kigoma kuuzwa katika Soko la Ulaya ambapo tayari kampuni moja ya Kitanzania imekwishaingia makubaliano ya kuuza tani 20 za dagaa kila mwezi nchini humo," ilieleza taarifa hiyo.

Aidha, taarifa hiyo ilieleza kuwa upatikanaji wa kibali ukikamilika, dagaa wa Kigoma watauzwa kwa wingi katika nchi mbalimbali za Ulaya kama ilivyo kwa minofu ya sangara.

Scanned with CamScanner

la muda wakati ikijipanga kujenga la kudumu.


Alisema wakati wanaendelea kusubiri hata la muda lililojengwa likawa halipitiki

chama hicho, hivyo akawataka wananchi hao kuwa wavumilivu wakati utekelezaji ukiendelea.

Alisema chama hicho kitahakikisha kinai-

na kwamba watasimamia ... linajengwa kulingana na thamani halisi ya fedha hizo.

NIPASHE UK16



Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Kimondo, Kata ya Igoma, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wakiogesha mifugo yao kwenye josho la kata hiyo, hivi karibuni baada ya kupewa dawa za kuogesha bure na Serikali. **PICHA: NEBART MSOKWA**

kutoa
di kuto
mafun
bila ku
kusaba
mawa
"Unde
kana
ili tun
mafun
kuta
imeku
mara
na ma
nanyi
aliser
Alisis
wa sh
lazim
omru
na kw
kali z
kwa
wasi
Baad
huria
wata
kazi
ria il
hatu

FAIDA

# Narco kuwatoza wafugaji Sh3,500 kwa ekari

**Dar es Salaam**. Ili kuhamasisha ufugaji wa kibiashara nchini, kampuni ya Ranchi za Taifa (Narco), imesema imeanza kutoza tozo moja kwa wawekezaji wote wanaohitaji ardhi.


Awali Narco ilikuwa na tozo za aina tatu ambazo ni Sh3,700, Sh5,000 au Sh7,000 kwa ekari kwa mwaka lakini sasa itakuwa Sh3,500.

Uamuzi huo ni utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli alilolitoa mwezi uliopita akiwa kwenye ziara wilayani Karagwe na kuigiza Narco kuwa na tozo moja.

"Tumekubaliana tuwe na tozo moja kuanzia leo kwa yeyote anayetaka kumiliki maeneo ya Narco kwa ajili ya kufuga," amesema Paul Kimiti, mwenyekiti wa bodi ya Narco.

Kampuni hiyo ina zaidi ya hekta 600,000 na kuanzia Februari mfugaji mwenye mkataba atatozwa Sh3,500.

"Mpango huu ni mzuri kwa sababu utawasaidia wengi kumiliki ardhi. Mwanzo wengi waliona kiwango ni kidogo ndiyo maana tuliweka tozo tofauti kwa makusudi na ukitaka eneo kubwa unatozwa zaidi lakini Rais akasema tuweke tozo moja," amesema.



Meneja masoko wa Narco, Mnzava Emmanuel amesema kwa tozo hiyo mpya, hakutakuwa na ubaguzi kati ya wawekezaji wakubwa na wadogo hivyo kuvutia wengi zaidi.

"Tozo ya nyama inayoingia nchini imeongezwa ili kuhamasisha wawekezaji wetu wa ndani. Ukiingia kwenye ufugaji wa kisasa na biashara soko lipo wazi, kote ndani na nje.

"Tunataka tuvutie ufugaji ili mchango wa sekta hii ukue badala ya kufuga kwa kuhamahama matokeo yake ukila nyama inakuwa kama misuli au kamba. Tunataka mtu akila asiumie taya, huu ndio ufugaji tunaotaka hivi sasa," amesema Emmanuel.

Amesema Narco inahitaji ushirika na wafugaji na kwa wadogo wanaweza kuungana mwenye ng'ombe wawili akawa na mwenzake kuomba ardhi.

TUJADILI UCHUMI
Pngowi2002@yahoo.com.
0 754 653 740
Aurea Simtowe
KONA YA MMACHINGA

Scanned with CamScanner